# Ngano na Elimu ya Kimagharibi: Mustakabali wa Ngano za Kinyankole katika Karne ya 21

Mukundane Benon[1], Magdaline Nakhumicha Wafula[2], and Nathan Oyori Ogechi[3]

[1]*Department of Kiswahili and Other African Languages, Moi University E-mail: bmukundane@kyu.ac.ug; ORCID: https://orcid.org/0009-0004-1315-0283*
[2]*Department of Kiswahili and Other African Languages, Moi University; E-mail: mnwafula@gmail.com; ORCID: https://orcid.org/0000-0001-9758-2315*
[3]*Department of Kiswahili and Other African Languages, Kisii University; E-mail: ogechinathan@gmail.com; ORCID: https://orcid.org/0009-0003-5726-5405*

APA Citation: Mukundane, B; Wafula M. N & Ogechi N. O (2025). Ngano na Elimu ya Kimagharibi: Mustakabali wa Ngano za Kinyankole katika Karne ya 21. *Ngano: The Journal of Eastern African Oral Literature,* 3, 99-116.

**Ikisiri**

*Makala hii inatokana na utafiti ambao tulifanya katika jamii ya Wanyankole kuhusu usimulizi wa ngano za Kinyankole kwa mikabala ya kiutendoneni na kiuamilifu. Katika utafiti huu, iligunduliwa kwamba ngano za Wanyankole zinaelekea kudidimia na kutoweka kabisa na wanalaumu elimu ya Kimagharibi. Kulingana na Wanyankole walioshuhudia jinsi mambo yalitendeka miaka kama sabini na zaidi iliyopita, usimulizi wa ngano ulikuwa nyenzo na fursa ya wanajamii kutagusana na kukuza hisia ya umoja na utambulisho wa kijamii. Ngano zao zilikuwa na majukumu mahsusi ambayo zilitekeleza katika harakati za kujamiisha wanajamii. Pamoja na hayo, ziliburudisha wanajamii papo hapo. Licha ya majukumu ambayo ngano hizi zilitekeleza na burudani ambayo zilitoa, zinaelekea kudidimia kwani, hazisimuliwi tena kama ilivyofanywa enzi za jadi. Je, ni kweli kwamba kudidimia kwa ngano zao kumesababishwa na elimu ya Kimagharibi? Ni kwa kiasi gani elimu hii imechangia kudidimia kwa ngano za Kinyankole? Wanyankole ambao mtafiti alikutana nao walionekana kupoteza matumaini wakilalamika kuwa usimulizi wa ngano zao huenda hautarudi kwa sababu mfumo wa elimu iliyopo hauna nafasi ya kuendeleza ngano zao. Je, kuna namna elimu inaweza kutumiwa kuendeleza ngano za Kinyankole? Haya ni baadhi ya maswali ambayo makala hii ilitazamia kujibu. Makala hii iliongozwa na nadharia ya uamilifu kama iliyoendelezwa na Malnowisk (1922) na kuboreshwa baadaye na Mesthrie na wenzake (2004). Makala hii imehitimisha kwamba elimu ya Kimagharibi imechangia kudidimia kwa ngano za Kinyankole. Matokeo ya makala hii yamechangia maarifa kuhusu jinsi elimu ya Kimagharibi inaweza kutumiwa kuhifadhi na kuendeleza ngano za Wanyankole.*

**Istilahi Muhimu:** *Wanyankole, Kinyankole, Elimu ya Kimagharibi, Kudidimia, Jamiisha*

## UTANGULIZI

Wanyankole ni kundi la Wabantu ambao wanaishi Kusini ya Magharibi mwa Uganda. Wanaishi katika jimbo la Ankole, katika wilaya za Bushenyi, Ibanda, Isingiro, Kiruhura, Mbarara, Mitooma, Nsiika, Ntungamo, Rubiriizi, Rwampara, Sheema na sehemu za Rukungiri kama zinavyooneshwa katika ramani ifuatayo:





*Figure 1: Ramani inayoonesha wilaya za jimbo la Ankole (Asili: Mtandaoni)*

Kulingana na sensa ya kitaifa iliyofanywa mwaka wa 2014, jimbo la Ankole lilikuwa na watu milioni tatu nukta mbili wakati huo (Gazeti la Monitor la Ijumaa, tarehe 19 Agosti, 2022). Lugha inayotumiwa na Wanyankole ni Kinyankole. Kabila la Wanyankole linaundwa na makundi matatu ya watu; Bahima ambao wanafuga ng'ombe, Bairu ambao wanalima mashamba na Wakulima (peasants) ambao wanalima na kufuga ng'ombe (Oberg, 1938). Wanyankole wana imani zao, desturi na mila zinazowaongoza kudumisha amani na uhusiano mwema. Kwa mfano, wana amali ambazo wanaziheshimu na kuziendeleza. Baadhi ya amali hizo ni: ndoa, talaka, kuzaa na kulea watoto, kumtolea mtoto jina, kazi za ujima, matanga, wosia na urithi. Katika jamii ya Wanyankole, lilikuwa jukumu la wazazi na kila mwanajamii kuhakikisha kuwa watoto wa jamii hiyo wanakua wakiwa na maadili na nguvu za kufanya kazi. Hata hivyo, wazazi ndio walikuwa na jukumuu kubwa la kudhibiti maadili kwa watoto wao; kwa maana, maadili ya msingi huanzia nyumbani.

Kirindi (2008) anasema kuwa tangu zamani, wazazi wamekuwa wakifunza watoto wao kimasimulizi na kimatendo namna ya kutenda kazi na kuzingatia amali nyingine za jamii yao. Anaendelea kusema kuwa kulikuwa na njia kadhaa ambazo wanajamii walitumia kupitisha mafunzo kwa watoto wao. Kulingana naye, njia mojawapo ambayo walitumia ni ngano. Ngano hizi zilikuwa zikisimuliwa katika lugha ya Kinyankole wakati wa jioni baada ya kazi za mchana kutwa (Kyobutungi, 2012).

Wazee waliwasimulia vijana ngano kama njia ya kuwajamiisha katika jamii yao (Kyobutungi, 2012, Ntare, 2019, Kirindi, 2008, Okpewho, 1986). Kulingana na Insaidoo (2011), wazee wa jamii za jadi za Kiafrika walitumia ngano kufundishia vijana wao maadili na amali nyingine kama zilivyotarajiwa katika jamii yao. Mulokozi (2017) anaeleza kwamba ngano kwa kawaida husimuliwa na wazazi, walezi au mabibi/mababu kwa watoto au wajukuu wao kwa lengo la kuwapa mafunzo muhimu ya maisha, na wakati huo huo kuwaburudisha. Anasema shughuli hii hufanyika saa za jioni, baada ya kazi, wakati wanafamilia wakisubiri chajio kiive wapate kula na kulala.

Kadri ninavyojua, usimulizi wa ngano za Kinyankole ulikuwa turathi muhimu sana ya Wanyankole wa jadi ambayo iliimarisha pakubwa mshikamano wa kijamii ambao unaonekana kuwa umetetereka katika jamii yao ya kisasa. Ngano zao zinaendelea kudidimia, kwani

hazisimuliwi tena kama ilivyofanywa wakati wa jadi. Baadhi ya Wanyankole ambao mtafiti alitangamana nao walilaumu Elimu ya Kimagharibi kuwa ndiyo inadidimiza usimulizi wa ngano za jamii yao. Kudidimia na kupotea kwa ngano za Kinyankole hudhihirisha kuwa vizazi vya baadaye havitapokezwa maarifa kuhusu ngano za jamii yao. Kwa kuhakiki maoni yaliyotolewa na Wanyankole kuhusu uhusiano uliopo kati ya ngano za Kinyankole na elimu ya Kimagharibi, makala hii ililenga kuangazia mustakabali wa ngano za Kinyankole katika karne hii ya ishirini na moja ambapo elimu ya Kimagharibi imelaumiwa kudidimiza utamaduni wa Wanyankole ambao ulikuwepo na ulifunzwa kupitia elimu yao isiyo rasmi.

## HALI YA ELIMU ISIYO RASMI KATIKA JAMII YA WANYANKOLE

Elimu isiyo rasmi ni ile ambayo ilitokana na shughuli za jamii za kila siku zilizohusiana na familia, kazi na burudani. Katika elimu hii, wazee na watu wengine wazima ndio walifunza vijana jinsi ya kuishi katika jamii yao. Wazee ndio walikuwa walimu na madarasa yao yalikuwa ni kukusanyika nyumbani, chini ya miti, penye moto, mawindoni, malishoni au mahali popote palipofaa (Muhangi 2008).

Katika jamii nying za jadi nchini Uganda, hakukuwa na mfumo wa elimu kama uliopo sasa. Kulikuwa na ule ambao kwa sasa unarejelewa kama elimu isiyo rasmi (Ann, 1966). Jamii ya Wanyankole pia ilikuwa na aina hii ya elimu. Hakukuwa na taasisi za elimu, wala walimu mahsusi; hakukuwa mbao wala vitabu na kalamu bali watoto na vijana pamoja na wanajamii kwa jumla walifunzwa amali zote zilizotarajiwa na utamaduni wa jamii yao. Elimu ilitolewa na kila mwanajamii fulani ili kufunza vijana kuwa wanajamii waajibikaji na wanaokubalika katika jamii yao. (Fallers, 1968; Apter, 1967). Kina baba, mama na wahenga wengine kupitia methali, ngano na maagizo ya moja kwa moja wangefunza vijana majukumu yao katika jamii (Apter-*ashatajwa)*. Wakati mwingine jamii ingetumia adhabu kali kukanya vijana. Kwa mfano, Wanyankole walilani na kukana msichana ambaye alipata mimba kabla ya kuolewa (Kasfir, 1969). Hata hivyo, elimu hii haikujikita kwa maadili pekee bali kwa kazi za mikono na akili pia. Ili kuhimiza umoja na mshikamano wa jamii, utamaduni na historia ya jamii ingeendelea kurejelewa na kufunzwa (Ade, 1984; Cunningham, 1969). Mafunzo yao yalihusu utamaduni wao, kilimo, kuelewa hali ya anga, mienendo mizuri ya kijamii, bidii za kazi, usalama wa jamii, imani za jamii, na mengine. Mafunzo yao hayakupangwa kwa njia maalum kama ilivyo kwa elimu rasmi bali wakati wowote, watoto na vijana walijifunza kutoka kwa watu wakubwa. Mafunzo yalitolewa kupitia masimulizi ya mdomo au kimatendo, ambapo watoto na vijana waliiga kutoka kwa baba, mama, shangazi, ami, babu, nyanya au wahenga wa jamii hiyo (Apter- *ashatajwa*). Hawa ndio walikuwa walimu wa jamii.

Kulingana na Wanyankole tuliowahoji, elimu isiyo rasmi ilitolewa katika mikusnyiko ambayo ilifanywa nyumbani, chini ya miti, mahali penye moto, mashambani wakivuna wimbi, malishoni au mawindoni baada ya kuua mnyama na kukaa kujifariji. Elimu hii ilifunza watoto wa Kinyankole kukua na maadili, kuwa wabunifu, wenye kiwango cha juu cha kutafakari, wenye bidii ya kazi, ujasiri, wenye kujiheshimu na kuheshimu wengine. Kupitisha elimu hii, Wanyankole walitumia mbinu mbalimbali kama vile: methali, vitendawili, nyimbo za kitamaduni, mafumbo na ngano, miongoni mwa nyingine. Ngano, kama njia mojawapo ya kufunzia watoto na vijana utamaduni wa jamii yao, ilithaminiwa na Wanyankole kwa sababu ngano zilizosimuliwa zilitekeleza majukumu maalum ambayo yalisaidia katika kujamiisha vijana kwa kutenda yaliyotarajiwa na jamii yao. Licha ya hayo, usimulizi wa ngano za Kinyankole unaendelea kudidimia na kulingana na Wanyankole, kudidimia huku kumesababishwa na elimu ya Kimagharibi. Makala hii, kwa hiyo, imechunguza mchango wa Elimu ya Kimagharibi katika kudidimia kwa ngano za Wanyankole na jinsi elimu hii inaweza kutumiwa kuhifadhi na kuendeleza ngano za Kinyankole.

## NADHARIA

Uhakiki wa data katika makala hii uliongozwa na nadharia ya uamilifu kama ilivyoendelezwa na Malnowiski (1884-1942) na kuboreshwa baadaye na Mesthrie na wenzake (2004). Kutokana na mawazo ya Wanaanthropolojia hawa, jamii yoyote hujengwa na kudumishwa na asasi za kitamaduni ambazo husababisha utangamano na kuleta usawa katika hali mbalimbali za jamii hiyo. Nadharia hii inachunguza jinsi kipengele mahsusi cha utamaduni wa jamii kinasaidia katika kuendeleza jamii hiyo. Aidha inachunguza uhusiano uliopo baina ya sehemu moja ya jamii na jamii nzima. Kwa hiyo nadharia hii ilituongoza kuchunguza mchango wa kipengele cha ngano katika kujenga jamii ya Wanyankole. Ingawa nadharia hii ina mihimili mingi, makala hii iliongozwa na mihimili mitatu ambayo ni; (i) Utamaduni ambao unahusisha jinsi jamii inaishi (ii) Ujamiishaji unaoangazia jinsi watu wa jamii hujifunza utamaduni wa jamii yao (iii) Kaida ambayo ni mwongozo maalumu wa jinsi ya kutenda mambo katika jamii. Kwa hiyo, nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza dhima ya usimulizi wa ngano katika ujenzi wa jamii ya wanyankole. Aidha, ilimwelekeza mtafiti kuchambua asasi ya elimu katika kujenga jamii ya Wanyankole na kueleza jinsi mfumo wa elimu uliopo unaweza kuungana na kipengele cha ngano katika kukuza utamaduni wa jamii ya Wanyankole badala ya kuudidimiza.

## ASILI YA DATA

Data ya makala hii ni sehemu ya utafiti ambao mtafiti alifanya kuhusu usimulizi wa ngano za Kinyankole kwa mikabala ya kiutendoneni na kiuamilifu na ilipatikana nyanjani katika jamii ya Wanyankole. Watafitiwa waliotutolea data waliteuliwa katika baadhi ya vijiji vya wilaya tatu za Ibanda, Mbarara na Sheema. Watafitiwa waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji wa kimaksudi. Ili kuwafikia watafitiwa lengwa, tuliongozwa na mwanakijiji mmoja ambaye tulipewa na mwenyekiti wa kijiji hicho ili kutufikisha kwa watafitiwa tuliotaka. Data yenyewe ya makala hii ni maoni ya Wanyankole kuhusu ngano za Kinyankole na mchango wa elimu ya Kimagharibi katika kudidimiza usimulizi wa ngano hizo. Data ilipatikana kutoka kwa Wanyankole walio na umri wa miaka kati ya 60-86 na wale walio kati ya miaka 18 na 35. Sababu za kuteua watafitiwa hawa ni kwamba Wanyankole wa umri wa miaka kati ya 60-86 wana ujuzi wa kutosha kuhusu usimulizi wa ngano za Kinyankole. Wameshuhudia nyakati zote ambapo ngano zilikuwa zinasimuliwa na wakati wa sasa ambapo zinadidimia. Aidha, Wanyankole wa umri wa kati ya 18-35 walimsaidia mtafiti kuhakikisha ikiwa vijana wana au hawana ujuzi kuhusu usimulizi wa ngano. Hii ilimsaidia mtafiti kutambua mwanya uliopo kitamaduni kati ya wazee na vijana.

## MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Data ya makala hii ilipatikana kwa kutumia mbinu ya ukaguzi, mahojiano na uchunguzi shirikishi. Mtafiti alitumia mbinu ya ukaguzi kupata data kutoka kwa vijana. Mtafiti aliwaweka vijana katika vikundi na kuwashirikisha katika mijadala kuhusu ngano za Kinyankole. Katika mahojiano, mtafiti aliandaa dodoso ambazo alitumia nyanjani ili kumwongoza katika kuhoji watafitiwa wake. Mtafiti aliteua Watafitiwa wake kimaksudi na aliwafikia kwa kutumia njia mbili; kuelekezwa na mwenyeji wa kijiji hicho au kwa kutumia sampuli mkufu ambapo mtafitiwa mmoja alimwelekeza kwa mtafitiwa mwingine. Katika mbinu ya uchunguzi shirikishi, mtafiti alijiunga na wasikilizaji katika shughuli ya kuitikia wasimulizi walipokuwa wanasimulia ngano kama inavyoonyeshwa katika picha hapa chini:

*Picha zilizomo katika Makala hii zimetolewa kwa idhini ya watafitiwa wenyewe.*



*Figure 2: Picha 1*



*Figure 3: Picha 2*

Katika picha 1, mtafiti (katika nguo nyeupe) pamoja na baadhi ya wanakijiji cha Ruyonza-Nyabuhikye wilayani Ibanda wanaelezwa na bibi (aliyekaa chini) kuhusu ngano za Wanyankole. Baada ya maelezo, alitusimulia ngano mbili ambazo alijiamulia yeye mwenyewe. Katika picha ya 2, mzee (mwenye kofia) anaeleza kuhusu ngano za Kinyankole huku mtafiti akinakili mawazo aliyotolewa. Mtafitiwa huyu naye alipomaliza kutoa maelezo ya jumla kuhusu ngano, naye alitusimulia ngano moja.

## MITINDO ILIYOTUMIWA KATIKA USIMULIZI WA NGANO ZA KINYANKOLE

Muundo wa usimulizi wa ngano za Kinyankole ulichukua mkondo wa kuwa na msimulizi kwa upande mmoja na wasikilizaji kwa upande mwingine ambapo wasikilizaji walikuwa wainitikia kila msimulizi alipotua. Msimulizi ndiye alianza ifuatavyo:

> **Msimulizi:** *Mbaganire Mbaganire* (Niwasimulie niwasimulie)
> **Wasikilizaji:** *Tebere/ Hmm…hmm/ Eego* (Tusimulie, Naam, ndiyo), na hapo msimulizi angeanza.

Kauli ya msimulizi ya 'mbaganire mbaganire' ilitayarisha wasikilizaji kuitikia masimulizi yake. Nao kuitikia kwa kusema 'tebere' kulimdhihirishia msimulizi kwamba wasikilizaji walikuwa tayari kumsikiliza. Basi hapo angeanza masimulizi yake, nao wangeitikia kila alipotua. Jukumu la wasikilizaji katika ngano lilikuwa ni kusikiliza na kupata ujumbe na pia kuitikia msimulizi kila alipotua. Kuendelea kuitikia kwa wasikilizaji kulimdhihirishia msimulizi kuwa walikuwa makini wakimsikiliza.

Usimulizi ulitumia usemi wa taarifa kwa kiasi kikubwa na ulijaa mbinu kadhaa za kisanaa, kwa mfano, tashhisi, taswira, istiara, chuku na nyingine. Wakati mwingine, msimulizi alitumia usemi halisi huku akiiga sauti ya mhusika aliyekuwa anasimulia juu yake. Ngano nyingi ziliandamana na nyimbo ambazo zilijulikana kama 'ebitongyerero.' Hizi ziliimbwa kwa sauti zilizoibua hisia, mihemuko au furaha kutegemea aina ya ngano, maana sauti iliyotumiwa kuimba wimbo na athari ya wimbo kwa wasikilizaji ilitegemea ngano inayosimuliwa. Kwa kiasi kikubwa nyimbo hizi ndizo ziliibua mihemuko na kuwafanya wasikilizaji kububujikwa na machozi.

Kiutendaji, ngano zilizosimuliwa zilikuwa na mitindo ya usimulizi ambayo iliathiri wasikilizaji na kuwasababisha kuitika na kutenda jinsi zilifunza. Usimulizi wa ngano zao ulisababisha vitendo kutokana na athari zilizoibua miongoni mwa wasikilizaji. Kama Searle (1975) na Austin (1962) wanavyosema kwamba maneno hutenda, maneno yaliyotumiwa katika usimulizi wa ngano za Kinyankole yalitenda kwa sababu yaliathiri wasikilizaji na kuibua hisia, mihemuko na ari ya

kutenda kazi kwa bidii. Kwa mfano, katika ngano za *Nyanzira ya Kabaiji* na *Kishokye ky'omwishwa tohunga sho?* (Kefeeza, 2023), *Akaibo k'omunyanja* (Kashaija, 2023) na *Njuma na Njunju* (Jovulet, 2023), kitendo cha kina mama wa kambo kujaribu kuua mabinti zao wa kambo kinaibua mihemuko na hisia za chuki miongoni mwa wasikilizaji. Kinachoibua mihemuko na hisia hizo ni mitindo ya usimulizi na ujumbe uliomo katika ngano zilizosimuliwa. Katika ngano hizi, wasimulizi waliingiza nyimbo 'ebitongyerero' (beti za nyimbo zinaoingizwa katika usimulizi wa ngano na mara nyingi huwa zinarudiwarudiwa) ambazo waliimba kwa sauti za dhiki zenye unyonge na zinazoathiri hisia na huruma za wasikilizaji. Sauti hizi pamoja na ujumbe uliomo huibua mihemuko na kuwasababisha wasikilizaji kulia. Ingawa hali hii huwaathiri wasikilizaji kwa njia hasi, huchochea hisia za kuchukia unyanyasaji wa watoto wa kambo. Vijana wanakua wakichukia unyanyasaji wa aina hiyo na kuomba kutofikiwa na hali kama hiyo.

Aidha, usimulizi wa ngano za Kinyankole ulisheheni ujumbe ambao uliwahimiza wanajamii hasa vijana, kufanya kazi kwa bidii. Katika usimulizi wao, wasimulizi walitumia tamathali nyingi za usemi kama vile taswira, tashbihi, tashhisi, chuku, sadfa, na kadhalika ambazo zilibeba maana nzito ili wasikilizaji wapate kuelewa ujumbe uliomo. Maana zilizobebwa katika usimulizi wa ngano fulani ziliathiri wasikilizaji na kuwafanya waitikie kwa kutenda kama walivyofunzwa katika ngano. Aidha ziliwahimiza kutokata tamaa au kutarajia matokeo ya papo kwa hapo bali, wawe na subira, kwani, subira yavuta heri. Kwa mfano, katika ngano ya *Miyanda n'embwaye Rukamba* (Kapuupa, 2023), kijana Miyanda aliteseka maishani baada ya kifo cha wazazi wake. Hata hivyo, hili halikumkatisha tamaa bali lilimpa ujasiri wa kuendeleza utajiri wa marehemu babake akisaidiwa na mbwa wake *Rukamba* na ndume wake Rugondo. Katika ngano hii, Miyanda daima alivamiwa na wezi wa ng'ombe waliotaka kumwibia ng'ombe alioachiwa na babake lakini kwa ujasiri wake na kujiamini pamoja na kusaidiwa na Rugondo na Rukamba, aliwaua wote kila walipomvamia. Siku dadake alitoa siri ya nguvu zake ndipo wavamizi walimshinda Miyanda na kumwibia ng'ombe wote. Ujumbe uliomo katika ngano hii uliwaathiri wasikilizaji kwa kuwahimiza kuwa na ujasiri na kujiamini wakati wa kutenda kazi. Aidha, uliibua hisia za kukashifu usaliti na tabia ya kuwaamini watu usiowajua. Hii ni kwa sababu dadake Miyanda asingemwamini yule mwanamke na kumtolea siri ya nguvu za Miyanda, Miyanda asingeshindwa na kuibiwa ng'ombe wake.

## MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA NA NGANO ZA KINYANKOLE

Kutokana na maelezo ya watafitiwa ambao tuliwahoji, iligunduliwa kuwa katika jamii ya jadi ya Wanyankole, ngano zilithaminiwa sana. Wazee waliwasimulia vijana ngano na baadaye wangewaambia vijana nao kusimulia ngano, kama njia ya kuwafunza na kuwazoeza kusimulia ngano. Kwa sababu hii, vijana walijifunza kusimuliana ngano kutokana na mafunzo ya wazee. Kwa hiyo, watoto kwa vijana, wanawake kwa wanaume na mabibi kwa mababu walipenda kusimuliana ngano. Mara zote, ngano zilisimuliwa baada ya chajio ili kupitisha wakati wa kulala. Mara chache, ngano zilisimuliwa jioni kabla ya chajio kama njia ya kushughulisha watoto wasilale kabla ya kupata chajio. Siku ambako familia ingetembelewa na wageni, sehemu kubwa ya usiku huo ingechukuliwa na usimulizi wa ngano huku wageni na wenyeji wakisimuliana ngano kwa zamu. Kwa upande huo, ngano zilikuwa chombo cha kuburudisha wageni. Wakati mwingine, watoto wangewashurutisha wazazi kuwasimulia ngano kwa sababu ya kuzoea kusimuliwa ngano. Hii ni ishara kwamba watoto wa Ankole ya jadi walipenda kusimuliwa ngano. Kuwashughulisha watoto katika kusimulia ngano kuliwaandaa kuwa wasimulizi bora wa siku za baadaye, jambo ambalo lilisaidia kupitisha utamaduni huo kutoka kizazi hadi kingine. Hii ilikuwa njia mojawapo ya kujamiisha vijana kama inavyoelekezwa na mhimili wa pili wa nadharia ya kiuamilifu

unaoangazia 'Ujamiishaji unaoelekeza jinsi watu wa jamii hujifunza utamaduni wa jamii yao.' Kwa mijibu wa nadharia hii, ngano ni sehemu moja ya utamaduni wa Kinyankole iliyochangia kuwepo kwa utamaduni mzima. Utamaduni huu ulistahili kupitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Njia mojawapo ambayo ilitumiwa kupitisha usimulizi wa ngano kama sehemu ya utamaduni wao ni wazee kufunza vijana jinsi ya kusimulia ngano nao wakafunza watoto wao baadaye.

Usimulizi wa ngano za Wanyankole haikuwa shughuli ya mtu fulani au jinsia fulani au kundi fulani. Kila mtu aliyetaka kusimulia alikuwa na fursa ya kusimulia wengine ngano. Hata hivyo usimulizi mara nyingi ulifanywa na wanawake ingawa watoto wakati mwingine wangehusishwa na kujihusisha katika kusimulia ngano. Iligunduliwa nyanjani kuwa ilikuwa nadra kwa wanaume kujihusisha sana katika usimulizi wa ngano. Kulingana nao, wanaume walikuwa wamekusanyika kunywa pombe, bali si kusimulia ngano. Kwao, hiyo ilikuwa kazi ya wanawake. Aidha, ngano zililenga kwa kiasi kikubwa, kukuza maadili miongoni mwa vijana na wanawake ndio walitakiwa kufunza watoto maadili. Mtoto ambaye angekua na tabia mbaya angemtusisha mamake kama ulivyo msemo wao kwamba *omwana mubi ajumisa nyina* (Mtoto mbaya hutusisha mamake). Kiuamilifu, ngano zilizosimuliwa zilitekeleza majukumu mengi sana katika jamii yao kiasi kwamba vijana walikua wakithamini mafunzo ya ngano za jamii yao. Mifano ya majukumu yaliyotekelezwa na ngano za Kinyankole ni kama yafuatayo:

Kwanza, usimulizi wa ngano ulijamiisha watoto na vijana wa Kinyankole katika utamaduni wao. Hii iliwasaidia kukua wakijua mitindo ya usimulizi wa ngano ili siku za mbeleni, wawe wasimulizi hodari. Mafunzo yaliyomo katika ngano hizo yaliwafunza vijana mienendo, mila, desturi, maadili na amali nyingine za jamii yao. Hili linashabihiana na dai la Insaidoo (2011) kwamba katika jamii za jadi za Kiafrika, wazee walitumia ngano kufundishia maadili na amali za jamii zao. Wasomi wengine wenye wazo kama hili ni Senkoro (2011), Kyobutungi (2012), Mulokozi (2017) na Kirindi (2008). Kama inavyoelekezwa na mhimili wa nadharia ya uamilifu ambao unasisitiza ujamiishaji unaoangazia jinsi watu wa jamii hujifunza utamaduni wa jamii yao, ngano za Kinyankole zilisaidia katika kujamiisha vijana, kuwaajibisha na kuwaheshimisha jamii. Mhimili wa kaida ambayo ni mwongozo maalum wa jinsi ya kutenda mambo, unaafikiana na mawazo ya Kirindi (2008) kwamba jamii ya Wanyankole ilikiwa na utaratibu wa kuishi maisha ambao vijana walistahili kufuata ili kuwa wanajamii wenye maadili na heshima. Ukiukaji wa utaratibu huo ulihatarisha uhusiano wa wakiukaji na wanajamii wengine ambapo wakiukaji wangelaaniwa au kukanwa au kuadhibiwa vikali (Muhangi, 2008).

Kama inavyoelekezwa na mhimili hapo juu kwamba kila mwanajamii afuate kaida zinazoongoza jamii, ngano za Kinyankole zilihimiza vijana na watoto kuwa watiifu na wenye heshima kama ilivyotakiwa na utamaduni wa jamii yao. Mtafiti, akiwa nyanjani katika jamii ya Wanyankole, alithibitisha kuwa ngano za Kinyankole zilifunza vijana kufuata utaratibu fulani kwani, alisimuliwa ngano kadhaa ambazo ziliwashauri vijana kuheshimu watu wa kategoria zote; watoto, wazima, walemavu, maskini, na wengine. Ngano hizi zilikuza maadili na mienendo mizuri miongoni mwa wanajamii. Baadhi ya ngano ambazo mtafiti alisimuliwa zenye lengo la kutekeleza jukumu la kuadilisha wanajamii ni *Nyabwangu na Nyabucureera* (Jovia, 2023), *Runyonyi rwa Bamugamba nibagwa* (Kyamuresire, 2023) na *Karungi n'amayonza* (Atukunda, 2023).

Ngano za Wanyankole zilizingatia masuala mtambuka, kama vile, ulemavu, jinsia, na utunzaji mazingira. Watu walio na ulemavu kwenye miili yao walisawiriwa kama wenye uwezo wa kutenda chochote kitendwacho na wengine wasio na ulemavu. Wanawake vilevile walichorwa kuweza chochote kiwezwacho na wanaume au hata wenye uwezo zaidi ya wanaume. Kuna ngano nyingi ambazo mtafiti alisimuliwa na zinazingatia masuala mtambuka na mifano ni; Ngano ya *Burungi*

*bwa Rubaya* (Margret, 2023) ambayo inakweza kijana mwenye ulemavu wa mwili aliyeshinda mashindano ya kuoa binti mrembo. Binti huyu alitamaniwa na matajiri wengi lakini kijana mlemavu ndiye aliwashinda wote. Katika ngano ya *Nyamwongyerere ya Migombwa* (Kashaija, 2023), msichana Nyamwongyerere alikuwa mtoto wa kike mingoni mwa ndugu wanane wa kiume. Nyamwongyerere hakutengewa majukumu mahsusi kwa sababu ya jinsia yake bali alifanya kazi zote ambazo zilifanywa na kakaze. Kwa mfano, alikuwa na zamu ya kufuga ng'ombe kama kaka zake. Hakubaki nyumbani kupika au kuosha vyombo kwa sababu ya jinsia yake, bali alifanyishwa kazi kaka zake walizofanya. Katika ngano ya *Zebikiire n'orukooko* (Kazoora, 2023), mkewe Zebikiire ndiye aliokoa familia yao kutoka kwa jinyama (orukooko) ambalo lilitaka kuwala wote. Yeye Zebikiire alikuwa ameshakubali kuliwa na jinyama hilo kusingekuwa mkewe kutumia busara na kunusuru familia yao.

Aidha, ngano za Kinyankole zilihimiza vijana kufanya kazi kwa bidii. Wazazi walitumia ngano zenye mafunzo yanayohimiza utendaji kazi kukanya wale wenye uvivu na wsiopenda kufanya kazi. Utendaji kazi lilikuwa jukumu la kila mwanajamii kwa sababu kila mwanajamii alitakiwa kuwa mzalishaji chakula kama msemo wao ulivyokuwa kwamba *otakora tarya* (asiyefanya kazi hali). Hii ni njia mojawapo ya ujamiishaji wa vijana kama inavyosisitizwa na mhimili wa nadharia ya makala hii unaosisitiza suala la ujamiishaji unaoangazia jinsi watu wa jamii hujifunza utamaduni wa jamii yao. Kila kijana alistahili kuwa na bidii katika kazi. Kwa mfano, miongoni mwa ngano alizosimuliwa mtafiti, kulikuwa na ngano ambazo zilihimiza vijana wa kiume kufanya kazi kwa bidii ikiwa walitaka kuwa wanaume kamili au ikiwa walitaka kuoa wake wazuri. Walihimizwa kuwa na nguvu za kimwili na ujasiri wa hali ya juu ili kukumbana na changamoto za dunia. Kwa vijana wa kike, ngano ziliwafunza kuwa wafanyakazi wenye bidii kwa vile waume walitamani wake wenye bidii. Mifano ya ngano kama hizi ni ya *Kahiigi* (Kagarura, 2023) ambapo Kahiigi (mhusika mkuu) alipigana na simba na kumwua ili aoe msichana wa roho yake, *Akafunjo K'omunyanja* (Margret, 2023) ambapo kijana mmoja alihatarisha maisha yake ili kung'oa kile 'kifunjo' kilichokuwa kimeota katikati ya ziwa lenye kina. Katika ngano hii, mfalme alikuwa ameweka sheria kwamba yeyote aliyetaka kuoa binti yake ang'oe kile 'kifunjo' kilichokuwa kimeota katikati ya ziwa. Wanaume wote walishindwa ila tu mmoja aliyeamua kujitolea. Alijitahidi na kung'oa 'kifunjo' hicho na kuoa binti mrembo huyo.

Ngano za Wanyankole zilichangia kutatua migogoro ya kifamilia na kijamii kwa ujumla. Migogoro ya kifamilia ilidhihirika katika baadhi ya ngano zilizosimuliwa nyanjani. Mfano wa ngano za aina hii ni, *Kishokye kyomwishwa tohunga sho?* (Kefeza, 2023). Ngano hii inazungumzia mama wa kambo aliyeshurutisha mume wake kuua binti wa mke mwenza aliyepata nyumbani. Analazimisha mumewe (babake yule binti) kumwua ikiwa anataka kumwoa na ndivyo alifanya. Anamwua na kuoa yule mwanamke. Kwa bahati mbaya, ndoa yao haidumu, inasambaratika. Ngano za aina hii zilikemea wanafamilia na wanajamii ambao walisababisha mizozo katika familia na jamii kwa ujumla. Ngano ya *Kishokye ky'omwishwa tohunga sho?* inatoa somo kwa wanaume ambao wanafunikwa na mapenzi ya dharura na kutenda mambo kiholera bila kutafakari matokeo yake. Jukumu lake ni kutahadharisha wanaume wanaochukuliwa na mapenzi ya wanaojiita wapenzi bila kuhakiki malengo yao. Inadhamiria kudumisha amani na usalama katika familia na jamii kwa jumla. Katika ngano ya *Rwabyogamu rwa Rubaya* (Ndeeba, 2023), watoto wa Rwabyogamu wanaishi kwa kugombana na kuvurugana, karibu kuuana. Wanaoneana wivu na kuchukiana si haba, mpaka babao anawafanyia busara na kuwafanya wajirudie na kuwa na amani kati yao. Kwa upande huo, ngao za Wanyakole zilichangia kwa kutatua migogoro ya kifamilia na kijamii katika jamii ya Wanyankole.

Ngano za Kinyankole zilikuza na kuendeleza stadi za kimaisha ambazo zilikua na kudumu miongoni mwa vijana wa jamii hiyo. Mifano ya stadi hizo ni kama kutafakari, kujiamini, utatuzi wa matatizo, ujasiri na mawasiliano bora. Katika baadhi ya ngano za Kinyankole, kulijitokeza hali na visa ambavyo vilikuwa hatari kwa maisha ya mtu. Hungeweza kufikiri kwamba kungetokea suluhisho ya tatizo kama hilo. Lakini, mhusika mkuu katika ngano ya aina hiyo alifikiria na kutafakari sana na baadaye kupata suluhisho kwa tatizo hilo. Mifano ya ngano za aina hiyo ni *Zebikiire n'orukooko* (Kazoora, 2023), *Wakame na Warugwe*, (Ndeeba, 2023), *Akafunjo k'omunyaja* (Margret, ashatajwa), na nyingine nyingi.

## USIMULIZI WA NGANO KATIKA JAMII YA WANYANKOLE YA KARNE YA 21

Katika jamii ya Wanyankole ya karne hii ya 21, ngano hazisimuliwi kama zilivyosimuliwa enzi za jadi. Wanyankole wenyewe wanalaumu elimu ya kimagharibi na usasa ambao wamerejelea kama "omurembe gwa dot.com" (enzi ya kidigitali).

Ingawa katika Ankole ya jadi ngano za Kinyankole zilithaminiwa sana na kusimuliwa daima kwa sababu ya majukumu ziliyotenda, zimeendelea kudidimia sana katika jamii ya sasa ya Wanyankole. Kutokana na maoni ya Wanyankole waliohojiwa, ngano hazisimuliwi tena jinsi zilivyosimuliwa enzi za jadi na kulingana nao, sababu mojawapo ambayo imechangia sana kudidimia kwa ngano zao ni elimu ya Kimagharibi. Miongoni mwa Wanyankole 54 waliohojiwa, 2 pekee ndio walisema bado wanawasimulia ngano wajukuu wao wakati wakiwa likizoni. 52 walisema kwamba hawasimulii ngano tena kwa sababu wale ambao wangekuwa wanazisimulilia, yaani, vijana na watoto, wanakuwa shuleni wakati wote. Walisema kwamba nyumbani kunakuwa na watu wawili au wachache ambao hawana hamu ya kusimuliana ngano. Isitoshe, wengi wao wamezisahau, hawazikumbuki tena. Wengi waliona aibu kuwa hawakumbuki ngano zao kama mmoja wao alivyosema;

> *"Hata naona aibu kuwa sikumbuki ngano yoyote! Mametu alikuwa anatusimulia ngano kila mara na ngano alizotusimulia nilikuwa nazijua zote. Inashangaza kwamba sikumbuki hata moja….na hizo ngano zilikuwa zinatusaidia kwa njia nyingi sana. Kwa mfano, sisi wasichana tulikua tukijua ni hatari msichana kutembea peke yake bila mtu wa kuandamana naye. Tangu wakati huo hadi wa sasa, siwezi kutembea peke yangu hasa wakati wa jioni au nikiwa naenda mbali na nyumbani kwetu…"*

Kutokana na maneno yake, ni dhahiri kwamba Wanyankole wanakosa usimulizi wa ngano, si kwa kupenda kwao, lakini kwa hali ambayo hawana uwezo kuibadilisha.

Kutokana na sampuli ya Wanyankole iliyohojiwa kugundua ikiwa vijana, watoto au wajukuu wao wanajua kusimulia ngano, 46 walikiri kuwa vijana wao hawajui kusimulia ngano kwa sababu hawazijui na wanazipuuza. Wazee walisema kuwa hata wao wakitaka kuwasimulia ngano, wao vijana huwapuuzia mbili wakisema kwamba hayo ya ngano yalipitwa na wakati. Hata hivyo, kuna wale waliosema kwamba watoto wao wanasema kuwa shuleni wanafundishwa kusimulia ngano. Ili kuhakikisha ikiwa ni kweli kwamba watoto wanafundishwa kusimulia ngano shuleni, tuliwahoji vijana wawili wa shule za msingi tuliobahatika kupata nyumbani na wakakiri kwamba wanafundishwa ngano za Kinyankole shuleni. Pia kuna nyanya wawili waliosema kwamba wao husimulia wajukuu wao wakija kijijini kwa likizo.



*Figure 4: Kijana wa kiume (chini) akisimulia ngano*



*Figure 5: Kijana wa kike (madoadoa) akisimulia ngano*

Kijana wa kiume alisimulia ngano aliyojifunza kutoka shuleni ilhali yule wa kike alisimulia ngano aliyosimuliwa na nyanyake. Kutokana na kusimulia kwao, tulitambua tofauti kubwa kati ya usimulizi wao. Yule wa kiume alisimulia ngano fupi sana, yenye wahusika wenye majina ya kisasa, kwa mfano alitumia jina *Gift* na *Oscar* kama wahusika wa ngano yake. Katika ngano yake, hamkuwa maudhui au mafunzo yaliyojitokeza moja kwa moja.

Kwa upande wa kijana wa kike, ngano yake ilikuwa ndefu kiasi na yenye majina ya kijamii na yenye maana kulingana na muktadha. Ngano yake ilitumia majina kama *Nyabwangu* (Msichana mwenye upupa) na *Nyabucureera* (Msichana mwenye upole). Ngano yake ilikuwa na mafunzo ya kutahadharisha watoto wa kike wenye upupa na kuwakanya kuwa na maadili.

Kwa muhtasari, usimulizi wa ngano katika jamii ya sasa ya Wanyankole hautiliwi maanani kama ilivyokuwa enzi za jadi. Mabibi na mababu, wazazi na walezi hawasimulii ngano kwa sababu hawana wa kusimulilia. Wanasema watoto na vijana ambao wangekuwa wanasimulilia wanakuwa shuleni mar azote na wakifika nyumbani, huwa wanakuja na kazi za shuleni za kufanyia nyumbani. Wakati wasipikuwa wanafanya kazi zao za shuleni, huwa wanakuwa kwa runinga, filamu au mitandao ya kijamii kwenye simu.

Elimu ya Kimagharibi, katika muktadha huu, ni elimu rasmi ambayo inafundishwa shuleni katika nchi zinazoendelea hasa za Kiafrika. Watafitiwa tuliowahoji walisema elimu ya kimagharibi ambayo baadhi yao walisema ya kisasa imeendelea kumaliza mambo ya kitamaduni ambayo Wanyankole walienzi sana, mfano mojawapo ukiwa ni usimulizi wa ngano. Walisema kwamba wazazi hawana nafasi ya kutangamana na watoto wao ili wawasimulie ngano. Hii ni kwa sababu wakati wote, watoto wanakuwa shuleni na huko hawasimuliwi ngano kwa sababu usimulizi wa ngano hautiliwi maanani. Kwa sababu hiyo, wanalaumu elimu. Kwa muda mfupi ambapo watoto wanakuwa nyumbani, huwa hawana muda wa kusimuliwa ngano kwa sababu wanakuwa wanafanya kazi walizopewa shuleni kufanyia nyumbani. Wengine wanakuwa kwa mitandao ya kijamii kwenye simu au kwa filamu kwenye televisheni. Wazazi walisema kwamba wakijaribu kuwashawishi kuwasimulia ngano, wao husema ya kwamba hayo ya ngano yalipitwa na wakati. Kwa upande huo, wanalaumu usasa. Kutokana na miktadha hiyo miwili, ni dhahiri kwamba kwa kiasi fulani, elimu ya kimagharibi na usasa vimechangia kudidimia kwa usimulizi wa ngano za Kinyankole kwa sababu vimewanyima watoto nafasi na fursa za kusimuliwa na kusimulia ngano.

## JAMII YA WANYANKOLE NA ELIMU RASMI YA KARNE YA 21

Kwa mujibu wa Kamusi ya karne 21, neno 'rasmi' ni ufuataji wa utaratibu au kaida zilizowekwa. Kwa hiyo elimu rasmi ni elimu inayofuata utaratibu au kaida zilizowekwa. Kulingana na Wikipedia https://sw.m.wikipedia.org, elimu rasmi ni njia ambayo hutumiwa kimaksudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Ni aina ya elimu/mafunzo ambayo yana mpangilio na utaratibu. Inafanyika darasani kutoka shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Chini ya aina hii ya elimu, wanafunzi hufundishwa ujuzi wa msingi wa kitaaluma. Baadhi ya sifa za elimu rasmi ni kwamba imeundwa kwa utaratibu, yaani, kila kinachotendeka katika mchakato wa elimu kimepangwa. Hufuata mtaala maalum na wa maksudi. Katika mfumo huu, kunakuwa na vipimo vya kawaida vya kutathminia wanafunzi. Kiufafanuzi, elimu rasmi ni ile iliyopangwa kidaraja, kwa mpangilio maalum na kuenea kutoka shule za msingi hadi chuo kikuu. Elimu hii huwa inajumuisha programu au kozi zinazolenga mafunzo ya kiufundi na kitaaluma. Hutokea katika nafasi na wakati maalum na hutuzwa kwa vyeti au shahada. Ni mfumo wa elimu mbao umepangwa wenye ratiba, mipango ya masomo, sheria na kanuni. Huwa na mitaala inayokuzwa kutokana na mahitaji ya jamii. Yanayofunzwa hutathminiwa na matokeo hutolewa kuwa kipimo cha kupimia wale ambao wataendelea kwa ngazi ya juu. Hii ndiyo elimu ambayo katika makala hii inarejelewa kama elimu ya kimagharibi kwa sababu ililetwa na Wamishonari wa kizungu wakati wa ukoloni.

Kwa sasa, jamii ya Wanyankole inafuata mfumo wa elimu rasmi ulioko nchini Uganda kwa ujumla. Elimu nchini Uganda imekuwa ikibadilishwa na kuboreshwa ili kukidhi matakwa ya karne ya 21. Matakwa ya elimu ya karne ya 21 yamekuwa suala ibuka duniani ambapo nchi hasa zile zinazoendelea zinalenga kutoa wasomi ambao wana uwezo wa kuzalisha kazi, kuwa wabunifu na kutamaniwa katika soko la dunia (TISSA 2013). Mojawapo ya mabadiliko yaliyosisitizwa katika mtaala ni kufundisha watoto wa shule za msingi hasa wale katika madarasa ya chini na chekechea katika lugha za jamii zao (Government White Paper, 1992). Katika karne hii, mfumo wa elimu unatazamia kutoa wananchi wenye thamani na wanaozalisha maarifa mapya, wabunifu, watatuzi wa matatizo na wenye ujuzi na umilisi wa kutumia teknolojia. Ili kufikia hili, walimu wanahimizwa kutumia mbinu za kufundishia za karne hii zinazokuza milisi na stadi za kimaisha katika wanafunzi. Mbinu hizi zinamtarajia mwanafunzi kuwa ndiye analengwa katika mchakato mzima wa ufunzaji na ufunzwaji. Mwalimu anaangaliwa kama mwelekezi na mwezeshaji ambaye shughuli yake ni kumtolea visa na miktadha ambayo itamwezesha mwanafunzi kufikiria na kujitambulia maarifa mapya yeye mwenyewe (NCDC, 2014; NTP, 2019). Kwa msingi huu, mwalimu anastahili kuhudumia mwanafunzi bali si wanafunzi kwa sababu kila mwanafunzi ana kiwango chake cha uelewaji kilicho tofauti na cha mwingine. Katika muktadha wa ngano, kila mwanafunzi anastahili kupewa nafasi na muda wa kutosha wa kusimulia ngano. Mwalimu akitumia usampulishaji na kuhusisha wanafunzi wachache katika kusimulia ngano, atakuwa ananyima wengine nafasi ya kujifunza jinsi ya kusimulia ngano. Kwa hiyo, haifai kwa mwalimu huyo kuhitimisha kwamba wanafunzi wote wameelewa.

Katika mtaala wa NCDC (2014), mbinu ambazo zimependekezwa kufundishia ni zile ambazo zinahusisha kila mwanafunzi mkiwemo na wale wenye mahitaji maalumu. Aidha, matumizi ya vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanahimizwa. Mwalimu anashauriwa kuhimiza shughuli zinazoendeleza stadi za utafiti, ushirikiano, kutafakari, na nyingine miongoni mwa wanafunzi wake. Miongoni mwa malengo ya elimu ya karne ya 21, kulingana na NCDC (2014) ni:

- Kuwawezesha wanafunzi kuwa na maadili mema kwa kushirikiana na kujali watu wengine katika jamii.
- Kuendeleza utamaduni na maadili katika maisha ya wanafunzi.
- Kuwawezesha wanafunzi kuthamini na kulinda mazingira wakitumia maarifa ya sayansi na ya teknolojia.
- Kuendeleza uzalendo, umoja, utambuzi wa haki, wajibu wa kila mtu na utambuzi wa haja ya ushirikiano nchini.
- Kuendeleza hali ya kudumisha elimu na maendeleo.
- Kukuza stadi za utendaji za kujikimu maishani.
- Kukuza upendaji wa kazi pamoja na moyo wa kujitegemea mwenyewe.
- Kukuza uwezo wa kutumia mkabala wa kutafuta suluhisho katika hali mbalimbali za maisha.
- Kuendeleza nidhamu na tabia nzuri miongoni mwa wanafunzi ili wakikua wawe wananchi wenye nidhamu katika jamii yao.

Kiuhakiki, malengo ya elimu ya karne ya 21 yanaafikiana na mafunzo ya ngano za jadi za Kinyankole kwa sababu maudhui na mafunzo yaliyosisitizwa na ngano za Kinyankole yanajitokeza katika malengo haya. Changamoto iliyopo ni kwamba mitindo ya usimulizi, muda wa usimulizi na thamani iliyopewa ngano ndiyo hafifu sana. Muda ambao umetengewa fasihi simulizi kwenye mtaala wa kitaifa hautoshi kufundisha vipera vyote vya fasihi simulizi. Fasihi simulizi haijaliwi wala kusisitizwa bali wanafunzi na walimu wanajali masomo mengine ambayo wanachukulia kuwa yenye thamani. Kutothaminiwa kwake kunatokana na sababu mbili ambazo wahojiwa walitambua; Kwanza, hazitahiniwi mwishoni mwa ngazi ya shule ya msingi na hata kwa ngazi zinazofuata, hazitiliwi maanani. Pili, walimu wengi wa shule za msingi hawana ujuzi wa kutosha kuhusu ngano za Kinyankole. Kwa sababu hiyo wanaziacha na kufundisha vipera vingine kama vile, vitendawili na methali. Sababu za walimu kupendelea kufundisha methali na vitendawili kuliko ngano ni kwamba kuna maandishi mengi kuhusu methali na vitendawili ambapo walimu wanaweza kurejelea wanapofundisha. Maandishi kuhusu ngano za Kinyankole ni machache sana, jambo ambalo linawafanya walimu kuzipuuza.

## MCHANGO WA ELIMU YA KIMAGHARIBI KATIKA KUDIDIMIZA USIMULIZI WA NGANO ZA KINYANKOLE

Kama ilivyoelezwa hapo juu kwamba Wanyankole wanadai kuwa sababu kuu ya kudidimia kwa usimulizi wa ngano zao ni elimu ya kimagharibi, msisitizo wanauweka kwa kipengele cha utahini. Mtafitiwa mmoja ambaye amewahi kuwa mwalimu alitoa maelezo ya kina kwamba kutokana na mfumo wa elimu rasmi nchini Uganda na nchi nyingi zinazoendelea, utahini ndicho kipimo cha kukadiria ubora wa mwanafunzi masomoni. Huwa unafanywa ili kuamua ni nani bora zaidi masomoni ili aendelee kwa daraja la juu. Kwa sababu hii, kumeibuka mashindano ya kimasomo ambapo kila mwanafunzi na kila shule wanajaribu kwa uwezo wao kuona kuwa ndio bora zaidi katika mitihani kuliko wengine. Matokeo ya mashindano haya yamekuwa ni wizi wa mitihani, kufundisha wanafunzi zaidi ya muda uliopangwa kwenye ratiba, na kulaza watoto shuleni ili wafunzwe hata wakati wa usiku au asubuhi mapema. Wazazi nao wameingizwa katika mashindano haya kwa kuamua kuacha watoto wao walale shuleni ili wafunzwe sana wasije wakashindwa kupata alama nzuri. Kwa vile wakati wote watoto wanakuwa shuleni, wazazi hawapati fursa ya

kuwasimulia ngano na kuwafunza kuhusu utamaduni wao. Kule shuleni wanakokuwa mara nyingi, hawafunzwi kusimulia ngano kwa sababu hazitahiniwi mwishoni mwa ngazi hiyo ya elimu. Ni kwa msingi huo, Wanyankole wanadai kuwa elimu ya kimagharibi imechangia kudidimia kwa usimulizi wa ngano zao na kwa njia zifuatazo:

Kwanza kabisa, watoto wanaishi shuleni. Kwa hiyo, wazazi hawana nafasi ya kuwa nao nyumbani ili wawasimulie ngano wakati wa jioni. Hata wale ambao hawalali shuleni, hurudi nyumbani jioni sana wakiwa wamechoka. Isitoshe huwa wamerundikiwa kazi za kufanyia nyumbani. Mara tu, wanapofika nyumbani, mmoja kwa moja wanarudi katika vitabu vyao kufanya kazi walizopewa ili wasiadhibiwe kesho yake wakifika shuleni bila kazi hiyo. Wazazi wanalalamika kwamba watoto wao wakati mwingi wanakaa hadi saa sita usiku wakisoma au wakifanya kazi walizopewa shuleni. Kwao, hali kama hii haiwezeshi wazazi kusimulia watoto wao ngano. Nyanya mmoja alilalamika kuwa yeye huwa anataka kuwasimulia ngano kwa sababu anazipenda lakini anapowaita, wao humcheka na kumkejeli kuwa hayo ni ya waliopitwa na wakati. Badala yake, wanaenda kutazama runinga au kutazama mambo yao kwenye simu. Hoja hii ikiangaliwa na kuhakikiwa kwa makini inazua swali; kupotezea muda kwa runinga au mitandao ya kijamii kwa simu kunatokana na elimu ya kimagharibi au usasa uliotawaliwa na matumizi ya kompyuta?

Wanyankole waliohojiwa wanasema kuwa awali, shule za msingi zilikuwa zinafundisha watoto kazi za ufundi na kuwatolea elimu iliyokuza stadi zao za kimaisha na za kudumu (Generic skills). Mhojiwa mmoja alisikitika kuwa kazi za kiufundi ambazo walifundishwa wakiwa katika shule za msingi hazifundishwi tena. Alitoa mifano ya kazi ambazo walifunzwa; wasichana walishona vikapu huku wavulana wakitengeneza virago kutoka kwa mafunjo ambavyo walikalia darasani. Kazi hizi zilikuwa zinasisitizwa katika ngano walizosimuliwa nyumbani. Ngano zilipowahimiza kufanya kazi za mikono na baadaye kazi hizo zikafunzwa shuleni, watoto waliendelea kuweka thamani katka ngano zao. Kazi nyingine ambazo wanafunzi walifunzwa shuleni na ambazo zilikuwa zinajitokeza katika ngano ni kushona mikeka, kupalilia migomba, kufyeka majani, kupanda mbegu kama vile maharagwe na mahindi na kutandaza.

Pamoja na hayo, ngano, kama kipengele cha fasihi simulizi, kimewekwa kwenye mtaala wa shule za msingi pamoja na vipera vingine kama vile vitendawili, methali, nyimbo na vingine. Hiyo ingekuwa hatua nzuri ya kuendeleza usimulizi wa ngano. Changamoto iliyopo ni kwamba muda uliotengwa kwa fasihi simulizi ni mdogo sana, hautoshi. Mtaala umetenga vipindi viwili kila wiki, kila kimoja kikiwa na dakika 30 pekee. Muda huu hautoshi kwa kila mwanafunzi kupewa nafasi ya kusimulia ngano, mbali na vile vipera vingine. Iligunduliwa kuwa wanafunzi wanaobahatika kupata nafasi ya kusimulia ngano huwa hawazidi 8 na mwishoni mwa muhula, wanafunzi wasiozidi 24 huwa wameshiriki katika kusimulia ngano. Hii ni kwa sababu dakika 30 za kipindi kizima cha ngano huhusisha maelekezo na udhihirishaji wa mwalimu, usimulizi wa wale wanafunzi na mwishowe, maswali na majibu. Muda huu hauwapi wanafunzi wote kushiriki katika kusimulia ngano na wale wanaopewa nafasi, muda wa dakika mbili au tatu wanazopewa hautoshi kukuza vipawa vyao vya usimulizi wa ngano.

Kulingana na nyanya mmoja ambaye alistaafu ualimu, baadhi ya walimu wanaofunza wanafunzi usimulizi wa ngano hawazijui wao wenyewe. Kuthibitisha hili, nilizungumza kwenye simu na mwalimu mmoja wa darasa la kwanza wa shule fulani ili kuthibitisha dai hili. Mwalimu alisema, muda hautoshi kwa sababu wanafunzi huwa wengi darasani na vipera vya fasihi simulizi vya kushughulikiwa ni vingi. Alisema kila kipera kinaweza kushughulikiwa mara mbili au tatu kwa muhula. Nilipomwuliza ikiwa anawadhihirishia wanafunzi jinsi ya kusimulia nguo kwa kutoa mfano, alikiri kwamba yeye hajui ngano yoyote. Kwa hiyo, anatuma wanafunzi nyumbani

wasimuliwe ngano na wazazi au walezi wao, nao wakirudi shuleni, wasimulie zile ngano walizosimuliwa nyumbani. Alipoulizwa ikiwa ana uhakika kuwa kila mtoto ana mtu wa kumsimulia ngano nyumbani, alisema hana uhakika, ila wanaorudi bila ngano, huwa hawajalini bali anawambia kusikiliza wale walio nazo. Hii ni changamoto kubwa kwa sababu inawanyima fursa ya kushiriki katika shughuli ya kusimulia ngano na wanafunzi hujifunza zaidi kwa kushiriki na kutenda kama walivyoelekezwa, chambilecho na wanafalsafa wa elimu kwamba, ukisikia, unasahau, ukiona, unakumbuka na ukitenda, unaelewa.

## MATOKEO YA KUTOSIMULIWA KWA NGANO ZA KINYANKOLE KWA JAMII YA WANYANKOLE

Kulingana na Wanyankole ambao tulihoji, kabla ya elimu ya Kimagharibi na siku za mwanzomwanzo baada ya elimu ya kimagharibi kuanzishwa, ngano zilikuwa zinasimuliwa na ziliendelea kusimuliwa lakini muda ulivyopita, usimulizi ukaanza kudididimia. Kushindana kwa shule katika mitihani kulisababisha watoto kutokuwa na muda wa kufanya kazi nyingine isipokuwa, kuwa katika vitabu wakati wowote. Shule nyingi zilianzisha mfumo wa wanafunzi kulala shuleni. Hili lilitenga wazazi na watoto. Walikutana nao muda mfupi wa likizo. Muda huu pia haukufaa kwa kuwa watoto walikuwa wanafanya kazi walizopewa kutoka shuleni. Watoto walikosa mafunzo waliyokuwa wanafunzwa nyumbani na wazazi au walezi wao. Matokeo yakawa;

Watoto kupuuza utamaduni wao eti umepitwa na wakati. Wamekweza utamaduni wa kimagharibi ambao wanarejelea kama wa kisasa. Utamaduni wa Wanyankole umeendelea kufifia na kusipowekwa mikakati ya kubadilisha hali hii, utatoweka kabisa. Vijana hawajui majina halisi ya Kinyankole yaliyotumiwa enzi za jadi kama yale yaliyotumiwa katika ngano. Mbali na majina ya watu au wanyama yaliyotambulisha Wanyankole, kuna maneno na misamiati mingine ambayo ilitumiwa katika ngano na vijana na watoto hawajui. Mifano ya majina ya watu, kama Bayara, Kicunguro, Zebikiire, Bayoroba, Bwengye, n.k; ya wanyama na ndege kama Ishamba, Mareere, Ensigiramutente, Enyongarwizi, n.k; ya mitishamba na nyasi kama ekicuragyenyi, omuhoko, omuhuukye, omushorooza, n.k na misamiati ya kawaida ya vitu kama ekigagara, okusingorora, okujaba amate, n.k yote yamesahaulika. Misamiati kama hii ilijitokeza katika ngano mbalimbali zilizosimuliwa. Vijana hawayajui, kwa maana katika kizazi kijacho, misamiati mingi itasahaulika nah ii italemaza lugha ya Kinyankole.

Maadili yameporomoka. Watafitiwa tuliowahoji walisikitika kusema kuwa elimu na usasa vimeharibu maadili ya wanajamii; vimeharibu mambo yaliyodhibiti utamaduni wao. Walisema vijana hawana heshima tena kwa yeyote, wanavaa vibaya na kutenda mambo yanayoaibisha hadharani. Walisema wakati ngano zilikuwa zinasimuliwa, vitendo kama hivi vilikuwa vinakashifiwa na watoto walisikia na kuheshimu mafunzo yaliyotolewa katika ngano. Kupitia ngano, mienendo na maadili yaliyotarajiwa katika jamii yalipitishwa kwa kila mwanajamii. Wake waliheshimu waume wao, watoto waliheshimu wazazi na watu wengine waliokutana nao njiani, watoto walisaidia wakongwe, wanajamii walisaidiana, kila mwanajamii alikuwa mwajibikaji, amani na umoja vilitawala. Kudidimia kwa ngano kulikosesha mafunzo haya, jambo ambalo lilisababisha kuporomoka kwa maadili.

Viongozi wa baadhi ya shule wamechangia uharibifu wa maadili wakijaribu kuvutia wanafunzi wengi kutoka shule jirani kujiunga na shule zao. Wao wameshatambua mambo ambayo vijana wanapenda na moja kwa moja wameyaingiza shuleni, kwa mfano, mashindano ya urembo, densi za usiku shuleni na mengine. Mmoja wa wazazi katika shule moja ya msingi alikuwa ameenda

kumtembelea mtoto wake lakini kisa alichoshuhudia huko kilimchukiza sana na akanasa video ya kisa hicho ambapo mtoto wa kiume wa umri wa takribani miaka minane (picha ya mtoto na jina la shule vimehifadhiwa kwa sababu ya usiri) akaituma kwa mitandao ya kijamii. Kijana huyo alikuwa amevaa kama mhuni, nywele zimechakaa na suruali zilizochanika. Shule ilikuwa imeandaa keki, maua na mapambo mengine ili kijana huyo akichagua msichana ambaye alipenda, ampambe na pamoja wakate keki walishane, amkumbatie wacheze. Video hiyo ilipowekwa mitandaoni, watu walitoa mawazo, wengine mihemuko na wengine hasira. Mmoja aliandika hivi:

> *A whole headmaster allows this nonsense in a school compound! This education is killing our children! We are destroying the next generation.*
> ***Mkuu wa shule mwenyewe kukubali ushenzi huu katika shule! Elimu hii inaua watoto wetu. Tunaua kizazi kijacho. (TY)***

Visa kama hivi huibua hisia za vijana na kuwaathiri kimasomo. Badala ya kutafakari juu ya yale waliyoyasoma huwa wanakumbuka visa hivyo. Aidha mavazi na mapambo ambayo yanahusishwa katika visa huwa hayafai katika mandhari ya shule. Pale ambapo ngano zilikuwa zinakashifu visa na vitendo kama hivi, mazingira ya shuleni yanavipalilia. Kwa hiyo, kutosimilia ngano, kumesababisha watoto kupotoka kimaadili.

Wakati ambapo ngano zilikuwa zinasimuliwa, wivu, fitina na uovu wa aina yoyote ulikuwa unakashifiwa. Ngao zilitumia wahusika mbalimbali ambao walifikiwa na matatizo Fulani kutokana na uovu wao. Watoto walikua wakiogopa kutenda maovu. Kudidimia kwa usimulizi wa ngano, ambako kulingana na makala hii, kumesababishwa na elimu ya Kimagharibi, uovu umezidi. Watoto shuleni wanaibiana, baadhi ya wazazi wanaweka sumu katika vyakula vya watoto wa wenzao siku za kutembelea watoto shuleni, na kadhalika.

## JINSI YA KUTUMIA ELIMU YA KIMAGHARIBI KUENDELEZA USIMULIZI WA NGANO ZA KINYANKOLE

Elimu ya kimagharibi ndiyo elimu rasmi katika nchi nyingi za Kiafrika na inaangaliwa na wengi kama njia ya pekee ya kufikisha watu kwa maisha bora; njia ya kupata ajira, njia ya kustaarabika, njia ya kupata mke au mume mzuri na mengine. Kwa hiyo, ina msingi imara katika jamii za Kiafrika na duniani kote. Aidha ndiyo inaaminiwa kuwa njia ya kujipatia maarifa ya kisayansi ambayo yametawala dunia nzima. Kwa sababu hiyo, Waafrika wamekweza utamaduni wa wale walioleta elimu hiyo dhidi ya utamaduni wao kama Mnyankole mmoja alivyosema kwamba elimu imeharibu mambo hasa ya kitamaduni katika jamii zao. Vijana na hata wazima wameacha utamaduni wao na kukopa wa wale walioleta elimu rasmi. Utamaduni huu wanauita usasa. Wanapuuza utamaduni wao eti wao “wanaenda na usasa” Basi, ikiwa hatuwezi kubadilisha hali hii, inafaa tuitumie kuendeleza tamaduni zetu. Kwa hiyo, inawezekana Wanyankole kutumia elimu kuhifadhi na kuendeleza ngano za Kinyankole. Hili laweza kufanywa kwa njia zifuatazo:

Kulingana na watafitiwa waliohojiwa, watoto na vijana huchukua muda mwingi shuleni kuliko ule wa nyumbani. Hii hunyima wazazi na walezi nafasi ya kuwasimulia ngano. Kwa hiyo walimu wanaokuwa na watoto na vijana hao shuleni kwa muda mrefu sana wapange vipindi vya kutosha vya fasihi simulizi ili kila kipera kishughulikiwe ifaavyo. Kwa kufanya hivyo, watoto watajifunza mitindo ya kusimulia ngano na kupata mafunzo yanayotolewa na ngano hizo.

Iligunduliwa kuwa baadhi ya walimu wanaostahili kufunza watoto usimulizi wa ngano hawaujui wenyewe licha ya kuwa kuna vipindi vichache vya fasihi simulizi ambavyo vimewekwa kwenye ratiba ya masomo. Ili kuwezesha watoto kujifunza usimulizi wa ngano walimu wanaofundisha

fasihi simulizi waendelee kufanya utafiti kuhusu ngano ili wapate maarifa ya kutosha ya kufundisha watoto. Walimu wana nafasi kubwa ya kuendeleza usimulizi wa ngano kwa sababu wana muda mwingi sana na watoto. Wasifunze ngano kwa sababu somo limewekwa kwa ratiba bali wawafunze wakilenga kukuza umilisi, ufundi na vipawa vya watoto vya kusimulia ngano. Aidha wafunze ngano wakisisitiza yale mafunzo yanayosisitizwa na ngano. Ni jambo la kuaibisha kumkuta mwalimu anajaribu kufundisha ngano ambazo hazijui mwenyewe. Ufundishaji mzuri wa ngano kwa wanafunzi kunawawezesha kuzithamini na kutilia maanani mafunzo yanayojitokeza katika ngano hizo. Hili litawawezesha kuzihifadhi vichwani na Kimaandishi na mafunzo yaliyomo vilevile yatahifadhiwa vichwani na katika maandishi na kupokelewa na vizazi vya baadaye.

Kwa vile idadi kubwa ya wanyankole ni wale ambao wanajua kusoma na kuandika, na kwa vile wasimulizi wa ngano wanaendelea kutoweka, ni bora kutumia elimu kuziendeleza ngano zao kwa kuziandika ili ziendelee kusomwa. Iligunduliwa kuwa kuna maandishi machache sana kuhusu ngano za Kinyankole. Mifano ya maandishi yaliyopatikana ni kitabu cha *Emitwarize ya Wakami* cha Kesi Nganwa (1962) chenye ngano 26 zinazohusu Sungura na ujanja wake, *Fire Place Experiences* na *The Hidden Princess* vya Bishop Stuart University (2017) na (2012) mfululizo. Katika vitabu hivi, maelezo yaliyomo ni ya Kiingereza ila ngano zilizomo zimeandikwa kwa Kinyankole. Miongoni mwa ngano tulizosimuliwa nyanjani, hakuna moja inayojitokeza katika zile zilizoandikwa katika vitabu hivi. Hii ina maana kwamba kuna ngano nyingi za Kinyankole ambazo hazijaandikwa na huenda zitasahaulika zisipoandikwa. Kulingana na mawazo ya watafitiwa, vitabu vya ngano viendelee kuandikwa na kuwekwa maktabani na kwenye mitandao ya kijamii ili jamii ya wanaojua kusoma na kuandikwa ipate kuzisoma na kuziendeleza. Ingawa hili litakuwa kinyume cha hali halisi ya fasili ya dhana ya fasihi simulizi kwamba fasihi simulizi hupitishwa kutoka kizazi hadi kingine kwa masimulizi ya mdomo, itakuwa ndiyo njia ya hiari iliyobaki ya kuzihifadhia ngano kuliko kusahaulika kabisa. Ngano zitakuwa zinaendelezwa kupitia kwa njia ya mandishi ingawa njia hii haitaonyesha mitindo halisi ya usimulizi inayohusika, kwa mfano, 'ebitongyerero', miondoko, hisia, mihemuko na hali.

## HITIMISHO

Ngano za jamii ya Kinyankole zilikuwa na umuhimu mkubwa katika kujenga na kuadilisha jamii ya Wanyankole. Usimulizi wa ngano zao uliwaleta pamoja na kudumisha umoja kati yao na kukuza vijana kuwa wanajamii halisi. Ngano za Kinyankole zilihimiza vijana kufanya kazi kwa bidii ili waheshimiwe baada ya kufaulu. Hata hivyo, licha ya kuwa ngano za Kinyankole zilitenda majukumu mengi, zinaelekea kutoweka kwa sababu hazisimuliwi tena jinsi ilivyokuwa zamani na sababu mojawapo ambayo imechangia kutosimuliwa kwa ngano hizi ni elimu ya Kimagharibi kama ilivyojadiliwa hapo juu. Kutosimuliwa kwa ngano za Kinyankole kumeathiri jamii ya Wanyankole kwa njia hasi. Vijana wameharibika kimaadili ingawa inasemekana kuwa na baadhi ya watu wakuu nao wameharibika kimaadili kutokana na ukosefu wa mafunzo ambayo walifunzwa kupitia ngano. Hata hivyo, licha ya kwamba elimu ya kimagharibi imechangia kudidimia kwa usimulizi wa ngano za Kinyankole, kuna uwezekano wa kutumia elimu ii hii kuendeleza usimulizi wa ngano mradi walimu na waendelezaji mitaala wakiamua hivyo. Isipokuwa hivyo, ngano za Kinyankole zitatoweka miaka michache ijayo.

## MAREJELEO

Bishop Stuart University. (2012). *Fire Place Experience in Ankole*. Bishop Stuart University, Mbarara.

Bishop Stuart University. (2017). *The Hidden Princess*. Millennium Press Limited, Kampala.

Dundes, A. (1969). Folklore as a Mirror of Culture. *Elementary English*, *46*(4), 471-482. http://www.jstor.org/stable/41386525

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Finnegan, R. (1974). How Oral is Oral Literature? *Bulletin of the School of Oriental and African Studies.* University of London.

Insaidoo, K. A. (2011). *Moral Lessons in African Folktales.* Author House.

King'ei, K. na Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kirindi, G. N. P. (2008). *History and Culture of the Kingdom of Ankole.* Kampala: Fountain Publishers.

Labov, W. na Waletzky, J. (1967). Narrative Analysis: Oral Versions of Personal Experience. *Essays on the Verbal and Visual Arts* (Ed. J. Helm). Seattle: Univ. Washington Press.

Liu, Y., & Greenhill, P. (2021). Folktale Speech Acts and Linguistic Politeness in Wolfram Eberhard's. *Folktales of China. Western Folklore, 80(2),* 137-176. https://www.jstor.org/stable/27152304

Lorentzon, L. (2007). Is African Oral Literature Literature? *Research in African Literatures*, *38*(3), 1–12. http://www.jstor.org/stable/20109492.

Malinowski, B. (1954). Myth in Primitive Psychology. *Magic, Science and Religion*. New York: Garden City.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu,* Mwanza: Serengeti. Educational Publishers Ltd.

Mbarouk, M. A. (2015). *Athari za Teknolojia katika Ngano*. Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma http://hdl.handle.net/20.500.12661/971

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Murphy, W. (1978). *Oral Literature*.

Musa, T. M. (1969). *Folktales from Ankole*. Kampala: Milton Obote Foundation.

Mushengyezi, A. (2003). Rethinking Indigenous Media: Rituals, 'Talking'drums and Orality as Forms of Public Communication in Uganda. *Journal of African Cultural Studies*, *16*(1), 107-117.

Mushengyezi, A. (2007). From Orality to Literacy: Translating Traditional Ugandan Oral Forms into Texts for Children.

Mushengyezi, A. (2013). Oral Literature for Children: Rethinking Orality, Literacy, Performance, and Documentation Practices (Vol. 154). Rodopi.

Mushengyezi, A. (2017). Translating Ugandan Oral Literature for Children: Audience, Form and Social Relevance. *Form, and Social Relevance (May 25, 2017)*.

Nantare. (2019). A critical Analysis of Images of Women and Gender Roles in Ankole Proverbs and Folktales.

Nganwa, K. K. (1962). *Emitwarize ya Wakami.* Kampala: Fountain Publishers.

Ninsiima, M. (2021). *The Potential of Kinyankore Culture as a Tourism Product*. Entebbe: Nkumba University Press.

Oberg, K. (1938). Kinship Organization of the Banyankole. *Africa, 11*(2), 129-159.

Okombo na Nandwa. (1992). *Reflections on Theories and Methods in Oral Literature*. Dodoma: Zanzibar.

Okpewho, I. (1992). African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuity.

Okpewho, I. (2003). Oral Tradition: Do Storytellers Lie? *Journal of Folklore Research*, *40*(3), 215–232. http://www.jstor.org/stable/3814909

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi.* Nairobi: Focus Publication.

Williams, F. (1951). Ankole FolkTales. *Africa,* 21(1), 32-40. Doi: 10.2307/1156156.